Milele, ambapo utakuwa pamoja nami Milele na Milele!"



Mpendwa rafiki! Yesu alilipa gharama kwa ajili yako. Damu yake mwenyewe msaslabani pale Kalvari. Sasa hupaswi kamwe kuwa mtumwa wa shetani. Unaweza kumwita Yesu akae ndani yako akakuweka huru mbali na dhambi na hatia (Mt. 11:28). Atakujaza furaha, unaweza kuishi katika ushirika na Mungu katika ulimwengu huu na ule ujao!

Kwa nini usimwite Yesu aje katika maisha yako sasa hivi! Unaweza kusema maneno haya:

*Yesu, asante kwa kufa msalabani kwa ajili yangu. Nisafishe dhambi zangu zote. Niokoe toka kwa shetani na dhambi. Nifanye niwe makao yako. Wewe ni Bwana wangu… katika ulimwengu huu na ule ujao… Amen!*

Huenda utapenda kujua mengi zaidi kuhusu mpango huu wa Mungu wa Ukombozi kwa ajili yako. Tafadhali usisite kuwasiliana nasi. Tungependa sana kukutana na wewe ana kwa ana na kuongea nawe jinsi unavyoweza kukua kiroho.

Wako, Katika Jina la Yesu,
**SAJU JOHN MATHEW**
Tembelea: www.sjmathew.com

Rafiki mpendwa, tupo hapa ili kukusaidia wewe kuandaa maisha yako ya milele pamoja na Yesu. Usisite kuwasiliana nasi:

Tafadhali wasiliana nasi:
Simu:

Pastor Moses Magembe- +255 715 283819/ 784 283818
Capt. Siyame Paul- +255 767 359993
Barua pepe: gospeldsm@gmail.com
Gospel Campaign Centre, TAG Majumbasita,
P. O. Box 77313, Dar es Salaam
Tanzania, East Afrika.



# NDEGE MDOGO: ALIYEUZWA MILIONI 1

Mtu mmoja wa mitaani alikuwa akichezea ndege:

Haukuwa mchezo halali. Ebu na tuutazame kwa makini mchezo huu. Mtu huyu jeuri alikuwa akinyofoa kila unyoya wa huyo ndege mdogo. Kelele kubwa ya maumivu aliyotoa yule ndege haikuwa kitu wala haikuingia masikioni mwa mtu yule. Alikuwa akicheka na kuendelea kufuarahia kitendo chake cha kikatili.

"Hey, Unafanya nini?" mtu mmoja muungwana alimwuliza yule mtu..

Naye alijibu, "Je huoni kwamba ninatoa kila unyoya wa huyu ndege? Na inapompa maumivu makali sana, mimi nafurahia kilio chake chenye maumivu. Ninaye paka nyumbani kwangu, nikishamaliza manyoya yale yote nitamtupia paka wangu nimpendaye. Paka wangu atamla Yummy Yummy… Yule mtu mara akaanza kucheza pale mtaani!"

"Ndugu, mruhusu huyo ndege. Ndege wameumbwa kwa ajili ya kuruka, kweli?" Yule mtu muungwana aliongea kwa sauti ya upole!

"Umesema nini?" Yule mtu wa mitaani alimnung'unikia yule muungwana. Ndege wanaweza kuruka angani lakini nikisha mnasa na mtego wangu anakuwa mali yangu! Sasa mimi ndiye ninayeamua juu ya hatima yake Hehehe!

"Hiyo si jukumu lako.. Kama ukimuuza niko tayari kulipa gharama yoyote".

"Gharama yoyote? Unaweza kunilipa shilingi milioni moja?"

"Hmm… Yup! Imeshatendeka!"



Shilingi milioni moja kwa ajili ya ndege mdogo wa porini? Yule mtu muungwana alihesabu zile pesa na akamkabidhi

yule mtu mwenye ndege. Alishangaa sana…. Kila mmoja alishagaa?

Yule mtu muungwana akamchukua yule ndege akamfurahia, akaondoka na kumwachia yule ndege mdogo aende zake akiruka angani.

Hadithi hii inatukumbusha jambo fulani lililotokea katika ulimwengu usioonekana. Wewe na mimi tuliumbwa kwa mfano wa Mungu (Mwanzo 1:26-28). Tulikuwa huru kama ndege kufurahia uwepo wa Mungu. Tukamwasi Mungu na tukachagua kushuka chini (Mwanzo 3:1-10). Tukachagua anasa za dhambi na kuacha furaha ya kiroho katika uwepo wa Mungu. Ili kutosheleza matakwa ya mwili, tukatamani, tukawa na wivu, tukaiba, tukakufuru, tukawa wagomvi na hata wauaji. (Galatia 5:19-21). Hatukujua kwamba kila anasa ya dhambi ilikuwa mtego wa shetani ambao ulitunasa ndani ya wavu wake.


Tulipokuja kutambua utumwa huu tulikuwa tumeshachelewa sana!

Nilikuwa kitu cha kuchezea mikononi mwa shetani. Shetani alinitesa na hakukuwa na njia ya kutoka. Kilio changu kikafika masikioni (Kutoka 3:7-11) hadi penye shimo nilipoangukia na kufanywa mtumwa wa shetani.

Hey…Unafanya nini na mtu huyu? Yesu akamwuliza shetani. “Je huoni?” Shetani akachekelea kwa dharau. Hii ndivyo ninavyofanya na wanadamu wote. Ninawatesa, ninaondoa furaha yao, naharibu familia zao, kuwasababisha wafanye fujo mitaani, kupiga kelele, walewe, wafanye uasherati, kuwafanya wawe na hasira, wapigane, wauane, wajinyonge, kuwaaibisha, kuwatia hatiani na maumivu. Napenda kuwaona wakiangamia.

“Ndugu” Yule muungwana akamsogelea yule mtu. “Hmmm… Je unaweza kumuuza huyu ndege?”

“Kuuza?” Yule mtu wa mtaani akachanganyikiwa. “Kwa nini? Huyu si ndege wa kufugwa mwenye sauti nzuri… Ni ndege wa porini… alijibu katika hali ya jaziba…?



Yesu akasema, Hawa ni watu walioumbwa kwa mfano wa Mungu, unafanya nini nao?

“Oh! Hiyo ni hadithi ya zamani sana, “Shetani akasema, Mungu aliwaumba kwa ajili yake. Lakini walitamani….wakapenda anasa! Nikawapa kila walichokihitaji kwa ajili ya tamaa yao ya macho na tamaa ya mwili na kiburi cha uzima (1Yoh. 2:12-15).

Nikawanasa kwa dhambi na sasa ni wangu. Walijiuza wenyewe kwangu. Ni wa kwangu!” Shetani akacheka!

“Je unaweza kuwauza ili kwamba niweze kuwakomboa kwa ajili ya Mungu?” Yesu akauliza.

“Hey! Kwanini unataka kuwanunua? Unajua kuwa ni waasi. Ni wao wenyewe walimkataa Mungu na kunichagua mimi kuwa bwana wao. Pia sasa hawako katika sura waliyoumbwa nayo. Nimewafanya ukiwa tena utupu. Kwa nini unataka kuwakomboa?”

“Hilo siyo jukumu lako! Kama ukiwauza nitawanunua kwa gharama yoyote!”

“Gharama yoyote?” Shetani alikuwa akijiandaa kutamka (snip)! “Kwa hiyo nitakuambia gharama yangu….”Shetani akaja katika roho akasema, “Ni…ni… DAMU YAKO!”

Yesu akanitazama… Nikauona Upendo na rehema katika macho yake…: Na mara akasema, “IMEKWISHA!” (Yoh. 19:30).

Yesu ilibidi afe msalabani ili kunikomboa mimi kutoka dhambini na hukumu ya milele (Yoh. 3:16). “Kwa nini Yesu alikufa kwa ndege asiyefaa kama mimi?” Mara nyingi nimeuliza swali hili kwa Yesu, “Kwa nini ulilipa gharma kubwa kiasi hicho? Damu yako mwenyewe kwa ajili yangu?”

“Yesu akasema, “Ninakupenda mwanangu, “Siwezi kukuacha uingie jehanam. Nimekuumba uishi na mimi. Nataka wewe uwe makao yangu. Nakutaka wewe uweze kufurahia maisha yako katika ushirika na mimi hata katika ulimwengu huu. Na safari yako ikimalizika, nitakuchukua katika Mbingu ya